



MARAFIKI WA ULIMWENGU - (MU)

Amici del Mondo, World Friends Onlus, ni shirika lisilo la Kiserikali lililoanzishwa kunako mwaka 2000, na kusajiriwa kama Shirika lisio la kiserikali mwaka 2002. Tangu mwaka 2004 lilisajiriwa nchini Italia katika Jalada kuu la Mashirika yasiyo ya kiserikali na makao yake Makuu yako mjini Roma, nchini Italia. Lengo kuu la Shirika hili ni kusaidia juhudi za kumwendeleza mwanadamu kutoka kila pembe ya dunia, kwa kusaidia utekelezaji wa kanuni msingi za utu wa mwanadamu kama zilivyobainishwa kwenye Azimio la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu, kwa kutoa kipaumbele kwenye sekta ya afya, makazi na elimu. Marafiki wa Ulimwengu tangu mwaka 2002 wamekuwa wakifanya kazi zao nchini Kenya kama wafadhili, ingawa wajumbe wake wengi na waanzilishi ni watu wenye taaluma zao, watafiti, wafanyakazi katika sekta ya jamii na wengine ni wataamu wenye ujuzi wa muda mrefu huko. Tangu mwaka 2005, Shirika hili limesajiriwa nchini Kenya kama Shirika lisilo la Kiserikali la la misaada kimataifa.

KAZI ZETU

Marafiki wa Ulimwengu (MU) wanatekeleza shughuli zao katika nchi zinazoendelea kwa kusaidia utekelezaji wa miradi katika sekta mbali mbali za maisha Lakini vipaumbele vyetu ni katika mambo yafuatayo;

1. **Sekta ya Afya: Mjini na Vijini: (MU)** wanatekeleza wajibu wao kwa kuimarisha Jumuiya mahali ili kuboresha huduma za kiafya pamoja na kuanzisha huduma za kinga, kwa kulenga zaidi afya ya mtoto na mama, kinga dhidi ya virusui vya UKIMWI na elimu ya afya.
2. **Mafunzo, elimu na uwezeshaji: MU** inasaidia katika sekta ya elimu kwa kugharamia mafunzo ya kitaaluma ili kuwawezesha watu.
3. **Shughuli za kiuchumi: MU** inasaidia juhudi za vikundi vya wanawake na vijana katika utekelezaji utakaosaidia uzalishaji ili kuinua kipato cha wahusika.
4. **MU** utekeleza miradi yake moja kwa moja na wakati mwingine husaidia shughuli na miradi ya wadau, vyama visivyo vya kiserikali, vyama mbali mbali, wakala na taasisi rasmi wanaotumika kama wakala wetu wa **MU**. Miradi inayodhaminiwa na **MU** inamwelekekeo chanya wenye mabadiliko ya kudumu unaopania kuondokana nafalsafa ya utegemezi kwa muda murefu na hivyo kujiondoa taratibu kila mara msaada unapotolewa. Shirika hili linafanya kazi kwa karibu zaidi na Jamuiya mahalia, kwa kuendeleza ufundi na mafunzo ya kitaaluma kwa ajili ya wafanyakazi mahalia na walengwa wa miradi hii. Jumuiya mahalia zinahusika



kikamilifu katika kusimamia na kutoa tathmini ya miradi hii: tatumini ya mwisho ni muhimu ili kuweza daima kuboresha uwezo na tija ya misaada inayotolewa.

5. **Utaalamu** ni nyenzo msingi katika shughuli za **MU** Shirika hili huwatumia wafanyakazi wenye uwezo mkubwa kitaaluma na wenye uzoefu wa muda mrefu katika miradi ya maendeleo.

Barani Ulaya na Italia nchi waanilishi, **MU** inasaidia kuhamasisha uelewa na taarifa za sababu ya uwepu wa tofauti kubwa kati ya Nchi za Kaskazini na zile za Kusini katika ulimwengu huu kwa njia ya habari na mafunzo. Mwelekeo wa pekee ni kwa ajili ya elimu ya vijana, kwa njia ya mikakati inayohusisha shule na wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu. Nchi ambazo shughuli kubwa za shirika kufanyika ni KENYA na SENEGAL.